JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

(PO-RALG)

WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA (TARURA)

WAKALA WA BARABARA TANZANIA (TANROADS)

MPANGO WA MAENDELEO YA BARABARA KWA USHIRIKISHAJI WA JAMII NA UFUNGUAJI WA FURSA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI (P164920)

RASIMU YA MPANGO WA USHIRIKISHAJI WADAU (SEP)

DISEMBA, 2020

MUHTASARI WA KIUTENDAJI

Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unahusisha mchakato wa kuwahusisha wadau kwa lengo mahususi la kufikia matokeo ya pamoja. Hivi sasa, Mpango huu unatambuliwa kama mbinu ya msingi ya uwajibikaji kwa kuwa unaitaka asasi kuwahusisha wadau katika kubainisha, kuelewa na kuyashughulikia masuala mahususi ya mpango/mradi yanayoibuliwa na wadau kwa ajili ya kutolewa uamuzi, utekelezaji, na hivyo kuboresha utendaji wa mpango/mradi.

Lengo la Programu hii ni kuboresha upatikanaji wa barabara vijijini na kutoa fursa za ajira kwa wananchi katika maeneo ya vijijini yaliyochaguliwa na kujenga uwezo katika usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kujumuisha mbinu za ushirikishwaji wa jamii.

Mpango huu una vipengele vinne (4):

- Kipengele cha 1: Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Vijijini
- Kipengele cha 2: Uimarishaji wa Taasisi na Rasilimali Watu
- Kipengele cha 3: Uhusishwaji, Ushirikishwaji na Ulinzi wa Jamii
- Kipengele cha 4: Ushughulikiaji Matukio ya Dharura

Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) utasimamiwa na kutekelezwa na Timu inayoshughulikia Mazingira na Masuala ya Kijamii ya TARURA/TANROADS. Lengo la jumla la SEP ni kufafanua mchakato wa ushirikishaji wa wadau katika Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi, na utoaji wa taarifa na ushauri kwa umma. Aidha, Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unaorodhesha njia ambazo Mpango huu unatekeleza kwa mawakala (ambao ni TARURA na TANROADS), washauri na wakandarasi watawasiliana na wadau kuhusiana na mbinu zitakazotumiwa kuwaruhusu watu kuibua madukuduku yao na namna yatakavyoshughulikiwa.

Wadau hawa walioainishwa ni wale ambao wameathiriwa na/au vikundi vya wadau wanaopenda kushiriki pamoja na wawakilishi wao rasmi na wale wasio rasmi. Utambulishaji wa wadau chini ya Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi utazingatia kazi na majukumu waliyo nayo; na ushawishi/mapenzi yao kwa Mpango huu. Watu binafsi ambao wako katika hatari ya kuondolewa kwenye mradi-mdogo wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi watapewa uangalizi mahususi.
Wadau watakaoshirikishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi ni:

- Waathirika chanya – kundi la watu au taasisi ambazo zimeathiriwa na shughuli za ujenzi, kama vile mtu au jumuiya zilizoathiriwa na mradi.

- Waathirikaji hasi – huhusisha watu binafsi au taasisi ambazo zinapenda kujihusisha na ardhi ambayo iko ndani ya eneo la njia (RoW). Wengi wa wadau hawa ni wamiliki wa ardhi zenye majengo tayari au mashamba ambayo yataathiriwa kwa kupoteza ardhi, majengo, na mapato yao ya kiuchumi.
- Vikundi vingine vinavyopenda kujihusisha – kundi la watu au taasisi ambayo inapenda kujihusisha na ujenzi na inaweza kuunga mkono mradi, mamlaka za serikali za mtaa au zile za ngazi ya taifa, wanasiasa katika serikali za mtaa au wa ngazi ya taifa, mamlaka za kijadi, viongozi wa dini, mashirika ya umma yakiwamo yale yasiyo ya kiserikali.
- Watu binafsi waliobainishwa kuwa katika makundi maalumu wakiwamo watoto, wanawake, watu wenye ulemavu, wazee na vijana.

Utoaji wa taarifa na ushauri kwa wadau utafanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwamo majadiliano ya vikundi lengwa (kutegemeana na umri, jinsi, na kazi), usaili, watoataarifa mahususi, na baruapepe. Ushauri utatolewa kwa muda ambao ni utakaowafaa washiriki kwa kuzingatia uelewa wao na pia kwa kutumia lugha ya asili.

Maoni kutoka kwa wadau yatapokelewa na mawakala wanaoshughulikia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi kwa njia ya maandishi na mazungumzo (kwa kutumia boksi la maoni, viongozi wa serikali za mitaa, mikutano ya hadhara, usaili, n.k.). Timu itapitia maoni ya wadau na kutoa mrejesho wa maamuzi ya mwisho na muhtasari wa jinsi maoni hayo yalivyoshughulikiwa.

Ili kushughulikia malalamiko yanayohusiana na Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi kutoka kwa jamii na umma ulioathirika, Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko (GRM) ulio wazi utaundwa katika Mpango huu ambapo kutakuwa na mchakato rasmi wa kupokea, kutathmini na kushughulikia malalamiko hayo. Zitaundwa Kamati za Kushughulikia Malalamiko katika ngazi za vijiji, kata, wilaya, mikoa, na pia katika Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) ulio chini ya Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi. Kwa wafanyakazi ambao wameajiriwa na wakandarasi, wakandarasi wanaohusika watatakiwa kuandaa miongozo ya kushughulikia malalamiko kama hitaji la msingi la zabuni.

Waraka wa Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unaonesha mkakati na mpango wa utekelezaji kwa kuwahusisha wadau tangu mwanzo hadi mwisho wa mradi.

Hata hivyo, Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) ndio uti wa mgongo wa mafanikio thabiti na yenye ufanisi. Vilevile, huu ni waraka wa kudumu utakaokuwa ukifanyiwa

udurusu na kuboreshwa pale inapohitajika kila mwaka ili kuakisi ushiriki wa wadau kadiri mradi unavyoendelea na wadau wapya watajitokeza.